JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA MABADILIKO YA KATIBA

MWONGOZO KUHUSU MABARAZA YA KATIBA YA ASASI, TAASISI NA MAKUNDI YA WATU WENYE MALENGO YANAYOFANANA

1.0. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (3) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Tume inawajibu wa kuunda Mabaraza ya Katiba kwa ajili ya kupitia na kutoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba iliyoandaliwa na Tume. Muundo wa Mabaraza ya Katiba unapaswa kuzingatia mgawanyiko wa kijiografia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mabaraza ya Katiba yatawashirikisha na kuwakutanisha wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya wananchi katika jamii kwa lengo la kutoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba. Aidha, kifungu cha 17 (8) kinaeleza kuwa, isipokuwa kama mazingira yatahitaji vinginevyo, Tume itabuni utaratibu unaofanana ambao utatumika kila upande wa Muungano.

Kifungu cha 18 (6) kinaeleza aina nyingine ya Mabaraza ya Katiba. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, Tume inaweza kuruhusu Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwa Tume.

Kwa Msingi huo, Tume imeamua kuwa Mabaraza ya Katiba yatakuwa katika makundi mawili yafuatayo:-

1.1. Mabaraza ambayo Tume **itayasimamia** na kukusanya Maoni **(Mabaraza ya Katiba ya Wilaya – Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa).**

1.2. Mabaraza ambayo Tume **haitayasimamia.** Mabaraza hayo yatajisimamia yenyewe na kukusanya maoni yatakayowasilishwa kwenye Tume kwa mujibu wa maelekezo. **(Mabaraza ya Katiba ya**

Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana).

Mwongozo huu unaainisha Muundo, utaratibu na uendeshaji wa Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana.

2.0. MUUNDO NA UTARATIBU WA UENDESHAJI WA MABARAZA YA KATIBA YA ASASI, TAASISI NA MAKUNDI YA WATU WENYE MALENGO YANAYOFANANA

2.1. Muundo

Muundo wa Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana utategemea Katiba,Kanuni, Randama na "Charter" ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana husika.

Miongoni mwa Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yanayoweza kuunda Mabaraza ya Katiba ni kama vile:

2.1.1. Jumuiya ya Kidini.

2.1.2. Chama cha Siasa.

2.1.3. Asasi ya Kiraia.

2.1.4. Taasisi ya Elimu ya Juu.

2.1.5. Chama cha Wafanyakazi.

2.1.6. Chama cha Wakulima.

2.1.7. Chama cha Wafugaji.

2.1.8. Chama cha Wanahabari.

2.1.9. Baraza la Watoto.

2.1.10. Taasisi ya Wafanyabiashara.

2.1.11. Mabaraza ya Wanawake.

2.1.12. Taasisi ya Kitaaluma.

2.1.13. Baraza la Vijana.

2.1.14. Baraza la Wazee.

2.1.15. Jumuiya ya Kijamii (CBO).

2.1.16. Chama cha Waajiri.

2.1.17. Chama cha Wanasheria.

2.1.18. Umoja wa Watanzania waishio Nchi za Nje

2.1.19. Wizara, Idara na Taasisi za Serikali

2.1.20. Kundi au makundi ya watu wenye malengo yanayofanana.

2.1.21. Kundi au makundi ya watu wenye mahitaji maalum katika jamii.

Asasi, Taasisi na Makundi ya watu yenye Malengo yanayofanana yaliyoorodheshwa hapo juu ni kwa uchache. Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu yenye Malengo yanayofanana mengine yenye sifa na ambazo hazikutajwa, zinaweza pia kuwa Mabaraza ya Katiba, kwa kadri itakavyofaa.

2.2. Uendeshaji

Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yenye mfumo wa kiuendeshaji kuanzia ngazi ya chini hadi taifa, yataandaa utaratibu wa kukusanya maoni kuhusu Rasimu ya Katiba kutoka kwa wanachama wao na kuyawasilisha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kupitia ngazi ya taifa.

Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana ambayo hayana mfumo wa kiuendeshaji kuanzia ngazi za chini, yataendesha Mabaraza ya Katiba katika ngazi ya taifa na kuwasilisha maoni ya wanachama wao Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yenye mfumo wa uendeshaji kwenye ngazi za chini pekee yanaweza kukusanya maoni ya wanachama wao katika ngazi hizo na kuyawasilisha Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Ngazi hizo zinaweza kuwa ni Kijiji, Shehia, Kata, Wadi, Tarafa, Wilaya, Mkoa au Kanda.

Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yatajisimamia na kujiendesha yenyewe kwa kuzingatia Mwongozo huu na Sheria za nchi zilizopo. Mabaraza ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yanaweza kukusanyika na kujiendesha wakati wowote kuanzia tarehe 01 Juni, 2013.

Ratiba za mikutano ya Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye Malengo yanayofanana zitapangwa na Asasi, Taasisi au Makundi husika. **Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye Malengo Yanayofanana, yatagharimia taratibu zote za uendeshaji wa Mabaraza ya Katiba hayo.**

3.0. UTARATIBU WA KUTAMBUA MABARAZA YA KATIBA YA ASASI, TAASISI NA MAKUNDI YA WATU WENYE MALENGO YANAYOFANANA

Katika kuiwezesha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuratibu kwa ufanisi mchakato wa kukusanya maoni kuhusu Rasimu ya Katiba, kila Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yatakayounda Mabaraza ya Katiba itatoa taarifa ya maandishi ya kusudio la kuunda, kuendesha na kusimamia Mabaraza ya Katiba. Taarifa hiyo itawasilishwa katika Ofisi za Tume ya Mabadiliko ya Katiba moja kwa moja – Makao Makuu, Mtaa wa Ohio - Dar es salaam au Ofisi Ndogo Mtaa wa Kikwajuni Gofu Jengo la Mfuko wa Barabara Zanzibar. Taarifa pia inaweza kutolewa kwa anuani zifuatazo:

Tume ya Mabadiliko ya Katiba
S.L.P 1681
DAR ES SALAAM

Au

S.L.P 2775
ZANZIBAR

Au

kwa barua pepe: katibu@katiba.go.tz

4.0. UTARATIBU WA KUWASILISHA MAONI

Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yatajadili na kutoa maoni kuhusu Rasimu ya Katiba katika tarehe zitakazoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Maoni hayo yanaweza kuwasilishwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa njia ya randama, barua, andiko, muhtasari wa makubaliano, n.k.

Mwisho wa kupokea maoni ya kutoka Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya watu wenye Malengo yanayofanana itakuwa tarehe 31 Agosti, 2013.

5.0. WASHIRIKI WA MABARAZA YA KATIBA YA ASASI, TAASISI NA MAKUNDI YA WATU WENYE MALENGO YANAYOFANANA

Kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (4) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yatakuwa maalum kwa ajili, na yatahudhuriwa na Raia wa Tanzania ambao ndio pekee watakaoruhusiwa kutoa maoni kuhusu Rasimu ya Katiba.

Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya wanaweza pia kushiriki kama wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi au Makundi ya Watu wenye Malengo yanayofanana ili mradi ni wanachama wa Asasi, Taasisi au Makundi husika.

6.0. UZITO WA MAONI

Maoni yatakayokusanywa kutoka kwenye Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana yatakuwa na uzito ulio sawa na maoni yatakayokusanywa kutoka katika Mabaraza ya Katiba ya Wilaya yatakayoendeshwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

7.0. TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA

Mwongozo huu utaanza kutumika tarehe 01 Juni, 2013.



Joseph S. Warioba
Mwenyekiti
Tume ya Mabadiliko ya Katiba